JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS-TAMISEMI

NAMBA ZA SIMU

Mkuu wa shule 0714-696814
Makamu 0786762000
Matron.0767-036898

Shule ya Sekondari Dodoma
S.L.P. 32
DODOMA
Simu Na:0262321163
E mail: dodomaseko@yahoo.com

Kwa: MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI……...
……
S.L.P …….
……..

YAH: **KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI DODOMA KIDATO CHA TANO (V) MWAKA 2018/19**

1. Ninayo furaha kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari Dodoma kidato cha Tano mwaka 2018 kwa chaguo la……(tahasusi)
Shule itafunguliwa tarehe 02/07/2018,hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 30/06/2018. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 15/07/2018.

1.1:KUFIKA ILIPO SHULE:
Shule ipo karibu kabisa na kituo cha mabasi yaendayo mikoani. Kutoka kituoni kuingia katika eneo la shule ukiwa na mizigo au wakati wa usiku unaweza ukachukua taxi kwa gharama iliyozoeleka isiyozidi elfu tatu, kinyume chake unaweza ukatembea kwa miguu taratibu kwa mwendo wa takribani dakika tano utakuwa umeingia katika eneo la shule. Unapotoka nje ya kituo cha mabasi kuingia kwenye mviringo (keepleft) inayoingia kituoni hapo majengo ya shule yenye rangi ya hudhurungi yanaonekana mkono wako wa kulia kama unaposhika barabara ya Morogoro- Dar au kuelekea majengo ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

1.2: MAMBO MUHIMU YA KUFANYA
Pamoja na kukupongeza kwakufanikiwa kupata nafasi hii muhimu ya kujiunga na kidato cha tano ninachukua fursa hii kusisitiza yafuatayo:-

I. **Kusoma kwa makini** maelezo yote yaliyoko katika fomu hii ya kujiunga (Joining Instructions) ya shule hii na kutekeleza bila kisingizio maelekezo yote ili kuleta ufanisi wenye tija katika kukupatia elimu iliyo bora kwa muda wote wa masomo.
II. Dodoma Sekondari ni shule ya Bweni kwa ajili ya **wasichana wote kidato cha Tano na Sita tu**.

III. Kujaza fomu Na: 3 **(fomu ya afya)** ambayo lazima ijazwe na Daktari wa hospitali au kituo cha afya cha serikali na kuirudisha shuleni wakati wa kuripoti.

IV. Kujaza fomu Na: 1 (Fomu ya ahadi) yenye utaratibu na sheria za shule, Fomu hii isomwe **kwa makini** na ijazwe na mwanafunzi na mdhamini wa mwanafunzi ambaye atakuwa mzazi au mlezi wa mwanafunzi husika

V. Kujaza Fomu Na:2 kwa wanafunzi wa BWENI.

2:MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA
2.1 SARE YA SHULE

2.1.2 MAHITAJI MUHIMU KUHUSU SARE KWA WASICHANA.

Sare ya shule iliyo sahihi kwa wasichana,ni sketi ya blue nyeusi (**dark blue**) ya marinda ya kupanga na shati jeupe mikono mifupi, mzazi anashauriwa kumnunulia mwanae pair mbili (2).

I. Wanaovaa hijabu mashati yao ni mikono mirefu na **hijabu nyeupe** isiyo na urembo wa aina yoyote ya kuvaa sambamba na sare ya shule na sio vilemba au mitandio. Ni muhimu kuhakikisha juba inafunika kifua sambasamba na viwiko vya mikono.

II. Viatu vya rangi nyeusi **vya kufunga na kamba** na visiwe na visigino virefu

III. Viatu vijulikanavyo kama simpo vyenye kuacha sehemu ya miguu wazi haviruhusiwi kabisa kuvaliwa shuleni.

IV. Soksi ndefu nyeupe jozi mbili.

V. Kwa wale wenye matatizo ya kiafya walete vyeti na barua kutoka Hospitali ya serikali ili kuwasaidia walezi wao namna ya kukaa nao shuleni.

VI. Nguo za michezo fulana T-shrt ya kijani isiyo na maandishi na raba nyeusi na soksi za blue.

VII. Mzazi unashauriwa kumpatia mwanao mahitaji ya kutosha kwani hataruhusiwa kutoka nje ya shule kwa muda wote wa masomo.

VIII. Mzazi/mlezi pamoja na mwanafunzi wa Bweni wajaze fomu ***Na: 1,2 na 3*** nakurejesha shuleni

IX. Wanafunzi wa Bweni wawe na jozi mbili za sketi nyeusi zenye marinda ya kupanga na flana **nyekundu zisizo na marembo au maandishi yeyote** za kuvaa wakati wakiwa nje ya madarasa siyo suruali.

X. Wasichana wa Bweni waje na vitu vifuatavyo:-

- Chandarua(mosquito net)
- Shuka mbili za rangi ya light bluena blanketi.
- Foronya mbili za rangi blue na mto.
- Ndoo binafsi mbili za lita kumi.
- Vyombo vya kulia chakula
- Mwanafunzi asilete shuleni nguo za ziada ambazo hazijaidhinishwa kwa sababu hazitavaliwa wakati wowote shuleni na pia hakuna sehemu ya kuweka mizigo.
- Sweta la blue lenye v shingoni kwa ajili ya kuvaa wakiwa darasani.
- Suruali nyeusi 2 zisizobana na jaketi la **blue** lisilo na maandishi au urembo zitavaliwa usiku wakati wa preparation.
- NB:MWANAFUNZI ASIJE NA MIZIGO AU BEGI KUBWA KWA SABABU HAKUNA NAFASI YA KUHIFADHI. Aje na tranka moja tu.

XI. Wanaovaa hijabu wanaruhusiwa kuvaa hijabu nyeusi nje ya madarasa sambamba na flana nyekundu na **siyo khanga.**

XII. Ni marufuku mwanafunzi kutembelewa na wageni wasioidhinishwa na mzazi, wakati wote atakaokuwepo hapa shuleni. Mwanafunzi atakayekiuka agizo hili atarudishwa nyumbani kwa muda usiopungua wiki tatu na mzazi atakiri kumpokea mwanae, na kumrudisha shuleni mara atakapomaliza adhabu yake.Ni muhumu kwa mzazi/mlezi kutoa nafasi kwa walimu kufanya kazi zao bila usumbufu wa kumshirikisha mwanafunzi mambo yasiyo na tija kwake.siku ya kuwaona wanafunzi ni siku ya mahafari ya kidato cha sita na nne.

2.2. ADA NA MICHANGO YA SHULE

a) **Ada ya shule kwa mwaka** ni shilingi 70,000 kwa mwafunzi wa bweni (wasichana). Unaweza kulipa kiasi cha shilingi 35,000 kwa mwanafunzi wa bweni (wasichana) kwa nusu muhula au kulipa ada yote mara moja.

b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi/mlezi ni:-

I. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani.
II. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha
III. Shilingi 30,000/= kwa ajili ya taaluma
IV. Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.
V. Shilingi 2,000/= nembo ya shule
VI. Shilingi 15,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza Tsh 10,000/= na Bima ya afya Tsh 5,000/=
VII. Shilingi 20,000/= mitihani ya kujipima mock
VIII. Shilingi 10,000/= kukodisha godoro kwa muhula.
IX. Fedha ya tahadhari Tsh.10,000/= (haitarejeshwa)

ANGALIZO: Jumla ya ada na michango kwa wanafunzi ni shilingi 213,000/=

N.B. Malipo yote ***ADA NA MICHANGO MINGINE*** ilipwe kwenye akaunti ya shule katika benki ya ***NMB .jina la account DODOMA SEKONDARI RUZUKU ACCOUNT***

Namba 5051100160 na risiti (bank pay in slip) iletwe Shuleni.(Tafadhari andika jina la mwafunzi kwenye pay in slip)
Mchango wa godoro ilipwe kwenye akaunti namba 50510009171

(c) Mahitaji muhimu ambayo ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

1. Mwanafunzi aje na vifaa vifuatavyo:-

Fyekeo 1, Reki 1, jembe 1 na mifagio ya nje na ndani kwa ajili ya kufanyia usafi (kwa mwaka)

2. Utatakiwa kuleta ***Rimu mbili (2)*** ya karatasi ya photocopy na sio ***Rulled wala Duplicating papers(kwa mwaka)***
3. Vifaa vya kujifunzia vya kutosha kama vile ***Madaftari, kalamu, vitabu na scientific calculators kwa wanafunzi wa sayansi na hisabati.***
4. Wanafunzi wa Biologia ***CBG*** na ***PCB*** waje na seti ya Dissection Kit kwa ajili ya mazoezi ya upasuaji ***Dissections.***
5. Mwanafunzi hatatakiwa kuja na mizigo isiyotakiwa shuleni. ***Soma kwa makini mahitaji ya mwanafunzi wa Hosteli***.
6. Ieleweke kuwa ni **marufuku kuja na simu shulen**i, na mwanafunzi atakayekamatwa na simu atafukuzwa shule.
7. Mwanafunzi atatakiwa kuleta picha za paspoti size tatu (3) akiwa na sare ya shule atakapokuwa ameripoti shuleni.(andika jina na tahasusi nyuma)
8. Begi kwa ajili ya kubebea madaftari.

. **(d) Upatikanaji wa vifaa na mahitaji muhimu**

Vifaa na mahitaji mengine ya mhimu yanapatikana katika duka lililoko shuleni kama ifuatavyo:-

i. Madaftari, peni, penseli, rimu za karatasi na Scientific calculator na Dissection kit vinaweza kupatikana duka lililoko shuleni.
ii. Masweta ya shule ya rangi ya bluu, yanapatikana hapa shuleni kwa bei nafuu katika duka la shule
iii. Huduma ya stationary
iv. Kuna kantini ndogo inayowapatia wanafunzi vitafunwa kwa wakati wakiwepo shuleni.
v. Wanafunzi wa Hosteli hupata huduma zote za malazi na chakula kwa muda wote wanaokuwepo shuleni.

2.3.TANBIHI: SHERIA ZA SHULE.

2.3.1 RATIBA YA SHULE.

Kila mwanafunzi azingatie kwa makini ratiba ya shule kwa kuwa mahali panapohusika kwa wakati muafaka. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa shuleni kuanzia saa moja na robo asubuhi kila siku kwa siku za masomo na kufanya yafuatayo:-

a) Kufanya usafi katika eneo lake alilopangiwa (special area)
b) Awahi mstarini (parade) na kuchukuliwamahudhurio mapema kengele inapolia, wachelewaji watashughulikiwa ipasavyo na walimu watakaokuwa zamu.
c) Kuingia darasani na kuhudhuria vipindi vyote kama vilivyo katika ratiba ya shule.
d) Ni lazima na sio hiari kwa mwanafunzi kufanya mazoezi yote yanayotolewa ndani na nje ya darasa

e) Kutii na kuheshimu kengele kwa kuwa mahali panapohusika kwa wakati mwafaka.

2.3.2 MATUMIZI YA SARE ZA SHULE

A. Kila mwanafunzi atatakiwa kuwa katika sare ya shule kama ilivyoainishwa katika fomu ya kujiunga na shule(Joining Instruction)
B. Wakati wa michezo wanafunzi wote watakuwa katika sare kamili ya michezo wakati wa ushiriki wao katika michezo na siyo vinginevyo.
C. Wanafunzi wa hosteli wawe na sare kamili wakati wakiwa nje ya madarasa, mwanafunzi atakaekutwa akiwa hana sare husika atapewa adhabu kali.
D. Wanafunzi wanaruhusiwa kuvaa sweta za rangi ya bluu, majaketi ***hayataruhusiwa***
E. Wanafunzi wa Bweni wavae sare kamili wanaposafiri kwenda likizo au wanaporudi kutoka likizo.

2.3.3 NIDHAMU

a) Ni marufuku mwanafunzi kutoka nje ya shule bila ruhusa ya mwalimu wa zamu, wanafunzi wa Bweni ruhusa ya kutoka nje ya shule itatolewa na matron, patron au Mkuu wa Shule.
b) Ni marufuku wanafunzi kukatiza uzio “tracepassing” katika njia isiyoruhusiwa, wanafunzi wote watumie lango kuu kutoka na kuingia shuleni.
c) Ni marufuku mwanafunzi kuzurura nje wakati wa vipindi, wanafunzi watakaokuwa na private studies wanashauriwa kuwa maktaba, ukumbi au darasa maalum litakalotengwa kama ukumbi wa shule utakuwa na matumizi mengine.
d) Ni marufuku kwa wanafunzi kuja na simu za mkononi shuleni.
e) Ni marufuku kupiga kelele wanapokuwa parade, darasani au katika private studies.
f) Ni marufuku kwa mwanafunzi kufuga ndevu,kucha, nywele na kusuka.
g) Mwanafunzi anapaswa kuwa nadhifu lakini haruhusiwi kutumia vipodozi kama wanja, lipshine, eyeshadow,cream n.k.
h) Wanafunzi wawapo shuleni, matibabu yao yatafanyika katika hospitali za umma.
i) Mwanafunzi awapo shuleni hatoruhusiwa kutoka nje ya shule ispokuwa siku maalumu (outing day na kwa ruhusa maalumu).
j) Kila mwanafunzi lazima ajue kuimba kwa ufasaha nyimbo zifuatazo:-
    - Wimbo wa “Taifa”
    - Wimbo wa “Tanzania nakupenda”
    - Wimbo wa “shule”.
    - Wimbo wa “Tazama ramani”
    - Wimbo wa “Kuwasha mwenge”

2.3.4 .SEHEMU AMBAZO WANAFUNZI HAWARUHUSIWI KUFIKA BILA KIBALI

- Chumba cha walimu (Staff room)
- Maabara
- Ofisi ya shule
- Jikoni, Hosteli ya jinsia tofauti
- Nyumba za walimu na wafanyakazi

2.3.5 SEHEMU ZILIZOPIGWA MARUFUKU WANAFUNZI KUTEMBELEA.

- Vilabu vya pombe
- Majumba ya starehe (Clubs)
- Nyumba za kulala wageni.

3.MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

Makosa yaliyoorodheshwa hapa chini yanasababisha mwanafunzi kufukuzwa shule moja kwa moja.

i. Wizi.
ii. Kutohudhuria shule masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/ utoro.
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana wanafunzi kwa wanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule.
vi. Kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu.
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
ix. Uvutaji wa sigara.
x. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuolewa.
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xiii. Kuwa mjamzito
xiv. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xvi. Kudharau Bendera na wimbo wa Taifa
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
xviii. Uhalibifu wa mali ya umma kwa makusudi
xix. Kukataa adhabu kwa kudharau au kwa kiburi
xx. Kukutwa nje ya shule bila ruhusa au kibali (Utoro)

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII YA DODOMA SEKONDARI

AMANI MFAUME

MKUU WA SHULE

FOMU NA. 1

(a) AHADI YA MZAZI / MLEZI

Mzazi / Mlezi anashauriwa kusoma kwa makini sheria na taratibu za shule pamoja na maelezo yaliyo katika form hii kabla ya kujaza sehemu hii na kuirudisha shuleni.

Mimi …….. wa ……

S.L.P. ……. Simu Na…… Mji ……

Ambaye kazi yangu ni …….. natamka hapa kama mzazi / mlezi wa ……

Ninakubali kwa hiari yangu mwanangu asome katika shule ya Sekondari Dodoma kuanzia tarehe ……ninaahidi kama ifuatavyo:-

1. Kwamba nimekubali chaguo alilopewa mwanangu na sitamruhusu kubadilisha hadi apate kibali cha maandishi kutoka kwa mamlaka husika.
2. Ninaahidi kumpatia mwanangu vifaa vyote kama vilivyoainishwa katika fomu ya kujiunga ikiwemo SARE KAMILI ya shule bila kuharibu chochote.
3. Ninatambua ya kuwa walimu wanahitaji ushirikiano wangu katika kumpatia mwanangu elimu na nitashirikiana nao bega kwa bega kwa maswala yanayomuhusu mwanangu kitaaluma na nidhamu ili aweze kufikia malengo yake nay a Taifa.
4. Naahidi kuwa endapo mwanangu ataenda kinyume na taratibu zilizoainishwa katika fomu hii achukuliwe hatua stahili za kinidhamu kama alivyoorodheshewa.

JINA LA MZAZI / MLEZI	**KAZI**	**SAINI**	**TAREHE**	**UHUSIANO**

AHADI YA MWANAFUNZI.

Mimi mwanafunzi ……

Wa kidato cha tano chaguo ……(tahasusi) mwaka 2017 / 2018.

Ninakiri kusoma, kuelewa na kuahidi kutii taratibu zote zilizoainishwa katila fomu iliyotumwa kwangu na Mkuu wa shule ya Sekondari Dodoma. Nitatoa ushirikiano wa kutosha kwa walimu wangu na shule kwa ujumla katika muda wangu wote nitakaokuwa shuleni ili niweze kupata elimu na kuendeleza jamii na taifa langu.

JINA LA MWANAFUNZI	CHAGUO	SAINI	TAREHE

Maoni ya Mkuu wa Shule …….

……

……

FOMU NA. 2: SEHEMU YA MZAZI

Mimi …….. wa ……

S.L.P. ……. Mji…….. Simu Na……

Nakiri kukaa na kuzungumza na mwanangu juu ya taratibu na sheria za shule na ninaahidi kumsaidia na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Mkuu wa Shule na walimu kwa muda wote ambao mwanangu atakapokuwa katika shule hii. Ninatambua madhara ya mwanangu kutembelewa na wageni wasioeleweka wakati akiwa shuleni na ninaomba shule iwatambue watu wanne(4) ambao wanahusika katika muda wote ambao atakuwa shuleni nao ni:-(ambatanisha picha passport size zao)

1. Jina ……. Simu…….. uhusiano…….
2. Jina ……. Simu…….. uhusiano…….
3. Jina ……. Simu…….. uhusiano…….
4. Jina ……. Simu…….. uhusiano…….

SAINI YA MZAZI ……Simu……

FORM Na. 3

Dodoma Secondary school

P.O. BOX 32

DODOMA.

MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by Medical Officer from a known Public Hospital or Health Centre in respect to all entrants

Full name …….. age ……
Sex ……year…….

1. Blood count (Red and White) ……..
2. Urine analysis Test …….
3. Syphilis test ……..
4. T.B. …….
5. Eye Test ……
6. Ears ……
7. Spleen …….
8. Abdomen …….

ADDITIONAL INFORMATION: eg. Physica impairment, family disease, chronic infections etc.

……
……
……
……

I certify that the above named individual is fit to pursue studies as stated above

…….. …….

Name and Designation Signature and Official stamp

…….. …….....

STATION DATE

NOTE:

1. Medical officer during the course of this Examination please attend the individual according to any diagnosed case.
2. The dully filled form must be handed to the Head of the School during registration week, under No circumstances should a student be registered without certification of his/her physical fitness.